



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

BEI YA MBOLEA YA RUZUKU KWA WAKULIMA

10 AGOSTI, 2022 – DAR ES SALAAM

Kutokana na kupanda kwa bei za mbolea katika soko la dunia na hapa nchini, Serikali imepanga na imetenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea itakayotolewa kwa wakulima wote nchini kwa lengo la kuwapunguzia makali ya bei. Mbolea zitakazohusika kwenye mpango wa ruzuku ni mbolea za kupandia na kukuzia kulingana na mahitaji ya soko.

Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea umezinduliwa rasmi na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 08/08/2022 jijini Mbeya katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima maarufu kama Nanenane. Katika uzinduzi wa mpago huo, Mhe. Rais alielekeza wakulima kuanza kununua mbolea kwa bei ya ruzuku ifikapo tarehe 15/08/2022.

Wastani wa bei za mbolea katika mpango wa ruzuku utakuwa ni kama ifuatavyo:-

AINA YA MBOLEA	WASTANI WA BEI YA MBOLEA BILA RUZUKU	BEI YA MBOLEA YA RUZUKU	RUZUKU YA SERIKALI
DAP	131,676	70,000	61,676
UREA	124,734	70,000	54,734
CAN	108,156	60,000	48,156
SA	82,852	50,000	32,852
NPKs	122,695	70,000	52,695

Aidha zoezi la usajili wa wakulima kwa ajili ya kunufaika na ruzuku iliyotolewa na Serikali unaendelea katika nchini kote.

Kwa mawasiliano tafadhali piga namba hii BURE 0733 800200.


Dkt. Stephan E. Ngailo
MKURUGENZI MTENDAJI



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022

Kilimo Street, Kilimo | Complex Building, P.O. Box 46238, 15471 Dar es salaam.
Tel: +255 22 2861939, E-mail: info@tfra.go.tz, Website: www.tfra.go.tz
All correspondence should be addressed to The Executive Director.